# TAMKO LA CHAMA CHA MAPINDUZI KWA AJILI YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2024





"Tumetekeleza, Kazi Iendelee...



"Tumetekeleza,
Kazi Iendelee...

**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi na
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# YALIYOMO.


1.0 UTANGULIZI uk.1

2.0 UHUSIANO WA SERIKALI ZA MITAA NA CHAMA CHA MAPINDUZI NA WANANCHI uk.5

3.0 UBORA, UWEZO NA UZOEFU WA CCM KATIKA KUTOA UONGOZI WA NCHI uk.7

4.0 MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI MKUU 2020-2025 uk.9

5.0 MAELEKEZO YA TAMKO KWA AJILI YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA MWAKA 2024 uk.11

6.0 HITIMISHO uk.33

# 1.0 UTANGULIZI

1.1 Mwaka 2024 ni mwaka wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika nchi yetu. Uchaguzi huu utahusu kuwapata Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji, Wajumbe wa Kamati za Mitaa na Wajumbe wa Halmashauri za vijiji. Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimeandaa tamko ambalo linaainisha ahadi na kutoa msimamo wa Chama katika kuwahudumia Wananchi. Tamko hili litakuwa ni dira kwa Wanachama wa CCM pamoja na Wananchi kwa ujumla katika kipindi chote cha mchakato mzima wa uchaguzi ikiwamo namna ya kupata viongozi bora na namna Serikali za Vijiji na kamati za Mitaa zitakavyotekeleza majukumu yake zitakapochaguliwa.

1.2 Tamko hili pia ni muongozo unaoainisha mambo muhimu yatakayozingatiwa na wagombea wa CCM katika Uchaguzi wa Viongozi wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji. Tamko limebainisha mafanikio ambayo Nchi imepata chini ya Uongozi wa CCM katika kipindi cha miaka mitano iliyopita na limeainisha maeneo ya kipaumbele ili kuhakikisha matarajio ya Wananchi katika nyanja zote yanafikiwa kupitia Serikali za Mitaa katika miaka mitano ijayo.

Lengo na umuhimu wa Tamko hili, ni kuainisha na kuelezea mafanikio yaliyofikiwa hadi sasa kwa baadhi ya sekta hususan za kiuchumi, kijamii na kisiasa chini ya utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Mwaka 2020 – 2025; na kuainisha fursa zilizopo na mikakati ya kuitumia kwa kushirikisha Wananchi wenyewe chini ya Uongozi wa Mamlaka zao. CCM inawaomba Watanzania wote waendelee kuiamini na kuwachagua wagombea wake ili kuendelea kuleta maendeleo kwa Wananchi katika maeneo yote ya nchi yetu. Ikumbukwe kuwa:-

(i) CCM inatambua haki na uhuru wa Wananchi katika kujiamulia mambo yao, hususan maendeleo yao ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Toleo la 2008, chini ya Ibara 145 (1), kupitia Bunge kwa upande wa Tanzania Bara na kupitia Baraza la Wawakilishi kwa upande wa Tanzania Zanzibar, imeanzisha mamlaka za Serikali za Mitaa katika kila Mkoa, Wilaya na maeneo ya Mijini na Vijijini;

(ii) Lengo la kuanzishwa Mamlaka hayo ni kuwapelekea wananchi wetu madaraka waliko ili waweze kutumia madaraka yao kukusanya mapato kwa maendeleo yao, kupanga mipango ya maendeleo, na kuitekeleza mipango kwa manufaa yao wote katika eneo linalohusika.

(iii) CCM itaendelea kuchochea uimara na ufanisi wa vyombo hivi muhimu vya madaraka na maendeleo ya wananchi wetu.

1.3 CCM inatambua kuwa Serikali za Mitaa sio tu ni miongoni mwa taasisi imara za Kidemokrasia bali pia ni kielelezo muhimu cha haki na uhuru wa Wananchi kuweza kushiriki katika shughuli za Utawala wa nchi yao ama moja kwa moja au kwa kuchagua wawakilishi wao kwa hiari, kila baada ya miaka mitano;

1.4 CCM imeshiriki katika chaguzi zote za mitaa za miaka ya nyuma na katika chaguzi hizo imekuwa ikipata ushindi wa kishindo.

Kwa namna ya kipekee, CCM inawashukuru kwa dhati Wanachama wake, Wapenzi na Wananchi wote kwa jumla, kwa kuendelea kuiamini na kuwachaguwa kwa kura nyingi za Ndio wagombea wa CCM katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; na

1.5 Kupitia tamko hili, CCM inawaomba na kuwasihi tena Watanzania wote, hususan walio na sifa za kupiga kura, kuendelea kuiamini na kuiunga mkono katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka huu 2024.

1.6 Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024 utaongozwa na Falsafa ya 4R iliyoasisiwa na Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, yenye ufupisho wa maneno manne (4) yafuatayo:-

i. **Reconciliation** (Maridhiano),
ii. **Resilience** (Ustahimilivu),
iii. **Reform** (Mabadiliko) na,
iv. **Rebuilding** (Kujenga upya)

1.7 Misingi ya Falsafa hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) CCM itaendelea kuzingatia umuhimu wa maridhiano katika jamii kwa kuhimiza kuishi kwa umoja, amani, utulivu na mshikamano.

(ii) Katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Mwaka 2024, CCM itazingatia kujenga jamii yenye Ustahimilivu, kwa kuhakikisha maelewano na mshikamano vinakuwepo na vinadumishwa bila kubaguana kidini, kisiasa, kikabila, kikanda, kiuchumi na katika kushiriki kwenye siasa na kudumisha demokrasia kwa kuimarisha Taasisi zinazosimamia haki jinai, haki za binadamu na usawa wa binadamu.

(iii) Kujenga Serikali za Mitaa ambazo msingi wake ni Mabadiliko chanya. CCM itaendelea kuzingatia kuwa maendeleo ya watu ndio kipaumbele cha kwanza; na kwamba Serikali za Mitaa zina kazi ya kufanikisha juhudi za pamoja za Wananchi katika kujiletea maendeleo.

(iv) Kudumisha utamaduni wa Kujenga upya fikra, tabia,mienendo na mifumo ili kuleta matokeo chanya katika maisha ya wananchi hususan nyanja zote za kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa manufaa ya wote.

(v) Kuhakikisha kwamba Serikali za Mitaa zinakuwa nyenzo za kuchochea juhudi za wananchi na kuwawezesha kiuchumi hasa katika matumizi ya sayansi na zana za kisasa za kutendea kazi kulingana na wakati uliopo ili kuboresha uzalishaji mali na utoaji wa huduma za jamii.

(vi) Kazi nyingine muhimu sana ya Serikali za Mitaa ni kuhakikisha kwamba mikopo ya asilimia 10 kwa Wana-wake, Vijana na Wenye ulemavu (empowernment) inatolewa, huduma za ugani kwa wakulima, wafugaji na wavuvi zinaboreshwa pamoja na kuwawezesha wachimbaji wadogo wa madini wapate dhana na mitaji. Pia kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kwenda shule wanaandikishwa na kusoma shule, wakiwemo wasichana na watu wenye ulemavu. Pia ni kuhakikisha kwamba wazee na wasiojiweza wanapata huduma bora za afya;

(vii) Kuhakikisha yanakuwepo matumizi yenye tija ya rasili-mali zilizopo ili kujenga uchumi imara na endelevu kwa maendeleo ya mtu mmoja mmoja, jamii na Taifa kwa ujumla ikiwamo nishati safi na uhifadhi wa mazingira; na

(viii) Kuimarisha misingi ya utawala bora katika Serikali za Mitaa. Hii itahusisha kuimarisha ushirikishwaji wa wana-nchi, uwazi na uwajibikaji wa viongozi, kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa na matumizi mabaya ya madaraka na rasilimali za umma.

(ix) Vikao vya Chama na vya Serikali za Mitaa vya ngazi husika vione kwamba utawala bora unazaa matunda tarajiwa katika kila ngazi.

# 2.0

# UHUSIANO WA SERIKALI ZA MITAA NA CHAMA CHA MAPINDUZI NA WANANCHI

2.1 Serikali za Mitaa ni nyenzo muhimu katika kuiwezesha Nchi kuwa na muunganiko wa Serikali Kuu na Mamlaka haya ili kurahisisha utekelezaji wa ahadi/Ilani inayolenga kuwahudumia Wananchi.



Hivyo, huduma bora kwa wananchi inategemea muunganiko na mshikamano wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa katika kutekeleza Ilani. Sambamba na hilo, ni mwendelezo wa Sera za CCM katika kuimarisha mifumo ya demokrasia kuanzia ngazi za Vitongoji, Vijiji na Mitaa hadi Taifa kwani mamlaka yote inatoka kwa Wananchi.

2.2 CCM inaziangalia na kuziona Serikali za Mitaa, kama:-

(i) Chombo cha Wananchi cha kuwashirikisha katika utawala wa umma;

(ii) Chombo cha kuwahamasisha, kuwasaidia na kuwawezesha wananchi kujiletea maendeleo yao ya kiuchumi na kijamii katika maeneo yao;

(iii) Kichocheo cha dhamira na jitihada za dhati za wananchi katika kupambana kupambana na umaskini miongoni mwa Kwa msingi wa kujitegemea huko huko waliko;

(iv) Nyenzo muhimu ya kuwawezesha Wananchi kupambana haraka na umasikini wa kieneo, badala ya kusubiri jukumu hilo kutekelezwa na Serikali Kuu pekee; na

(v) Chombo madhubuti cha kuendeleza matumizi endelevu ya rasilimali, katika kukuza uchumi na kuwajengea Wananchi uwezo wa kuzitambua na kuzitumia fursa zilizopo katika maeneo yao ili wajiletee maendeleo endelevu yao wenyewe katika nyanja zote za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni.

(vi) Katika ngazi zote za Uongozi na utawala, CCM haitakuwa legelege ili isizae Serikali legelege. Itasonga mbele daima, kwake kurudi nyuma ni mwiko.

# 3.0

# UBORA, UWEZO NA UZOEFU WA CCM KATIKA KUTOA UONGOZI WA NCHI

3.1 Tarehe 5 Februari, 2024 CCM imetimiza umri wa miaka 47 tangu kuzaliwa kwake, hapo tarehe 5 Februari, 1977. Kwa usuli na historia yake iliyotukuka, CCM ni miongoni mwa vyama vichache katika nchi za ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara vyenye uongozi bora, imara na wenye uzoefu wa muda mrefu katika kuongoza na kuwatumikia Wananchi kwa weledi na mafanikio.

3.2 Hivyo, mbali na kutekeleza lengo na madhumuni ya kuanzishwa kwake, kama ilivyoainishwa chini ya Ibara ya 5 (1) ya Katiba ya CCM, sababu nyingine za msingi

za CCM kushiriki katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024 na kuwaomba wananchi waendelee kuiamini na kuwachagua wagombea wake kwa kura nyingi za Ndio, ni hizi zifuatazo: -

(i) Ndicho Chama pekee hapa nchini chenye uzoefu usiotiliwa shaka wa Siasa, Itikadi na Sera nzuri zinazotekelezeka, zilizojengwa chini ya misingi imara ya kulinda na kuendeleza uhuru wa Taifa letu, haki, usawa, amani na maendeleo ya Wananchi wote;

(ii) Ndicho Chama chenye historia ya kupigania ukombozi wa Taifa letu, kuleta uhuru wa kweli, heshima, umoja, amani na mshikamano na kuleta Muungano wetu baina ya Tanganyika na Zanzibar na kuzaa Taifa jipya la Tanzania likipiga vita dhidi ya aina zote za ubaguzi wa kikabila, Jimbo, dini, rangi wala upendeleo wa kisiasa, kiuchumi, kimaendeleo na kiutamaduni.

(iii) Ndicho Chama chenye viongozi imara wenye uwezo na uzoefu wa kuongoza Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, kwa muda mrefu na kulifikisha Taifa letu kwenye mafanikio makubwa ya maendeleo ya Wananchi kijamii, kiuchumi na kisiasa;

(iv) Ndicho Chama chenye muundo na mtandao wa uongozi imara katika ngazi ya Kitongoji, Kijiji na Mtaa. Hivyo, kinazielewa na kuzifahamu vyema changamoto za wananchi na namna ya kuzipatia ufumbuzi wa kudumu huko huko wanakoishi, na;

(v) Ndicho Chama kilichopewa ridhaa na Wananchi, ya kuongoza Serikali zote mbili; Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kusimamia ipasavyo utekelezaji wa Ilani yake ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 – 2025, kwa pande zote mbili za muungano wetu.

# 4.0

# MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI MKUU 2020-2025

4.1 Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024, unafanyika ndani ya kipindi cha miaka minne (2020 – 2024) ya utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020 – 2025.

4.2 Ndani ya kipindi hicho, CCM chini ya Uongozi mahiri wa Dkt. Samia Suluhu Hassan,Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeweza kupiga hatua kubwa ya mafanikio katika sekta za maendeleo kwa Wananchi wa Tanzania.

4.3 Tamko hili limejikita kwenye mafanikio ya utekelezaji wa Ilani kwa Serikali za Mitaa. Aidha, Tamko hili lina maelekezo mahsusi yanayopaswa kuzingatiwa na wagombea wote katika uchaguzi huu wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024.

4.4 Tamko hili lina maelekezo makubwa matano (5) kama ifuatavyo;-

- *i.* *Mageuzi ya* ***Kiuchumi***
- *ii.* *Maendeleo ya* ***Watu***
- *iii.* *Utawala bora, haki,* ***ulinzi na usalama***
- *iv.* *Maendeleo ya sayansi,* ***teknolojia na uvumbuzi***
- *v.* *Mazingira na mabadiliko* ***ya tabianchi.***

# 5.0

# MAELEKEZO YA TAMKO KWA AJILI YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA MWAKA 2024

Kama ambavyo tumedokeza awali katika fungu la 4.4 hapo juu,Tamko hili lina maelekezo muhimu matano.Wagombea wote wa CCM katika Uchaguzi huu wa Serikali za Mitaa watatakiwa kuyazingatia kwa dhati.Ufafanuzi wa kila kipengele uko kama ifuatavyo;-

5.1 Mageuzi ya Kiuchumi

5.1.1 Tanzania imepiga hatua za maendeleo katika Nyanja za Kiuchumi. Baadhi ya maeneo hayo ni ujenzi wa miundombinu ya kisasa na uendelezaji wa sekta za kiuchumi, ujenzi wa barabara, reli, usafiri wa anga, kilimo, ufugaji na uvuvi, nishati, madini na ardhi.

Aidha, mageuzi makubwa yanayoendelea nchini yameimarisha uchumi wetu kutokana na hatua zilizochukuliwa katika kuimarisha utawala bora, kuchochea maendeleo ya sayansi na teknolojia, na kuwawezesha wananchi kiuchumi. Lengo ni kuongeza ajira na kupambana na umasikini. Baadhi ya mafanikio hayo ya kiuchumi ni haya yafuatayo: -


(a) Kuweka mazingira bora na wezeshi kwa wawekezaji wa ndani na nje. Jitihada hizi zimekuza kasi ya kukua kwa uchumi, kutengeneza fursa za ajira na kuinua ubora wa maisha ya wananchi. Mageuzi yaliyofanyika yanajumuisha: -

(i) Kuwawezesha Wananchi kiuchumi kwa kupunguza gharama za uzalishaji kwa kutoa ruzuku ya mbolea na mbegu pamoja na kuwapatia wakulima soko la uhakika lenye bei nzuri ya mazao ikiwemo kahawa, mahindi, mchele, ufuta, korosho na mbaazi. Aidha, stakabadhi ghalani, uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora za kilimo na mbari za mifugo na utoaji wa ruzuku za pembejeo (mbolea, viatilifu na zana za kisasa za kilimo);


(ii) Utoaji wa dawa za kuogeshea mifugo, chanjo na miundombinu ya masoko ya minada pamoja na uzalishaji wa malisho vimeinua vipato vya kaya nchini.

(iii) Kuwapatia wavuvi mikopo midogo midogo yenye riba na masharti nafuu ikihusisha boti za uvuvi, ufugaji kwa njia ya vizimba na kupambana na uvuvi haramu. Hatua hizi zimesaidia kupunguza umaskini wa kaya;

(b) Kutekelezwa kwa miradi mikubwa ya kimkakati yenye tija kwa maendeleo ya nchi yetu ukiwemo mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere Hydro-electrical Power Plant (JNHPP) na ujenzi wa reli ya kisasa (Standard Gauge Railway - SGR). Miradi hii imeleta fursa za ajira, kujipatia kipato kwa Wananchi na kuongeza tija na ufanisi katika shughuli zao za kiuchumi na kimaendeleo, kwa kuimarisha usafiri na usafirishaji. Vile vile, mradi huu wa JNHPP utaongeza kiasi cha umeme unaozalishwa nchini na hivyo kuleta uhakika wa upatikanaji wa nishati ya umeme na unafuu wa gharama za umeme utaongeza idadi ya kaya zenye huduma ya nishati ya umeme kwenye vijiji vyote vilivyounganishwa. Hadi sasa jumla ya Vijiji 5,481 vimesambaziwa umeme na kufanya jumla ya vijiji vyenye umeme kufikia 11,837 sawa na 96.37% ya Vijiji 12,318 vya Tanzania Bara. Aidha, gharama za uunganishaji wa umeme Vijijini zimepungua;



**(SGR)**
ujenzi wa reli ya kisasa




**(JNHPP)**
Julius Nyerere Hydroelectrical Power Plant

**UMEME** TANZANIA BARA.

**HADI SASA**

Vijiji **5,481**
vimesambaziwa umeme

Vijiji **11,837**
vina umeme





(c) Kujenga miundombinu ya matumizi ya gesi asilia na kuhamasisha matumizi yake viwandani, majumbani, kwenye taasisi na katika magari ili kupunguza gharama za nishati na uharibifu wa mazingira;

(d) Ujenzi wa barabara, madaraja na vivuko katika maeneo ya mijini na vijijini. Kwenye barabara za lami, urefu umeongezeka kutoka kilomita 86,472 mwaka 2020 hadi kilomita 91,532 mwaka 2023; na urefu wa barabara za changarawe umeongezeka kutoka kilomita 893.04 mwaka 2020 hadi kilomita 1042.43 mwaka 2023. Barabara hizi zimesaidia usafiri wa watu na usafirishaji wa bidhaa yakiwemo mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na bidhaa za viwandani na hivyo kuwaongezea wananchi kipato, kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna pamoja na kuongeza faida ya biashara kwa kupunguza muda wa usafirishaji wa mazao;

(e) Kupunguzwa na kuondolewa kwa utitiri wa tozo, ada na faini zilizokuwa zinasababisha kero kwa wakulima, wasafirishaji na wafanyabiashara ndogondogo. Aidha, taasisi zenye malengo yanayoshabihiana zimeunganishwa kuondoa muingiliano na kuongeza ufanisi katika kufanya biashara;

(f) Kutatua kero za wafanyabiashara wadogo kwa kuwatengea maeneo ya kufanyia shughuli zao katika Mikoa yote nchini;

**BARABARA**



**LAMI**
kutoka
**86,472** Km
mwaka
**2020**

hadi
**91,532** Km
2023




**CHANGARAWE**
kutoka
**893.04** Km
mwaka
**2020**

hadi
**1042.43** Km
2023

(g) Mikopo imetolewa kwa makundi ya Wananchi ili kuwajengea uwezo wa kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji na biashara. Mathalani, katika kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita jumla ya Shilingi Bilioni 245.95 zimetolewa kwa wanawake (24,373), vijana (13,873) na watu wenye ulemavu (5,305) kutokana na asilimia 10 ya mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa; na

| | |
|---|---|
| ***Miaka*** | **5** |
| ***Bilioni*** | **245.95** |
| *kwa vikundi vya* | |
| ***wanawake*** | **24,373** |
| ***vijana*** | **13,873** |
| ***Walemavu*** | **5,305** |

***KUTOKA***




*ya mapato ya ndani ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa*

(h) Kuwezesha wachimbaji wadogo kufanya shughuli zao kwa tija kwa kuwatengea maeneo, kuwapatia leseni, kuanzisha vituo vya mfano vya wachimbaji wadogo, kuwapa mafunzo ya uchimbaji, uchenjuaji na uongezaji thamani ya madini, kuanzisha na kuimarishwa masoko ya madini kufikia 42 mwezi Juni 2024, kudhibiti utoroshaji wa madini nje ya nchi na kuongeza ajira kwa makundi ya kijamii hasa vijana;

KUANZISHA NA KUIMARISHWA

**MASOKO YA MADINI**



kufikia

**42**

mpaka Juni **2024**

(i) Kuimarisha utalii kwa kulinda na kukuza vivutio vilivyopo vikiwemo maporomoko ya maji, milima, misitu, mazingira asilia, fukwe, malikale na hifadhi za wanyama. Kupitia mkakati wa Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa "Royal Tour", sekta ya utalii imestawi na kukua kwa kiwango kikubwa na kuongeza fedha za kigeni, kutengeneza ajira na kukuza pato la Taifa.

(j) Kuongezeka kwa jitihada za urasimishaji wa maeneo ya Vijiji ili kuondoa migogoro baina ya watumiaji ardhi. Katika kipindi cha 2021-2022 pekee vyeti vya ardhi ya kijiji 142, vimetolewa na hatimiliki 42,684 za kimila zimetolewa; na kuna hatimiliki 65,441 na hati za sehemu ya jengo 284 zimesajiliwa;

**Kati ya 2021-2022**



| | | |
|---|---|---|
| ***Vyeti*** *vya Ardhi ya Kijiji* | **142** | ***Vimetolewa*** |
| ***Hatimiliki*** *za Kimila* | **42,684** | ***Zimetolewa*** |
| *kuna* ***Hatimiliki*** | **65,441** | |
| ***Hati*** *za Sehemu ya Jengo* | **284** | ***Zimesajiliwa*** |

(k) Kuimarisha usimamizi wa Ardhi katika maeneo mbalimbali Nchini. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Novemba 2020 hadi Agosti 2024, Serikali imetekeleza masuala yafuatayo: -

(i) Kupima viwanja 1,416,037, mashamba 11,039, vijiji 891 katika maeneo mbalimbali nchini; pamoja na Kutafsiri na kupima mipaka ya kiutawala ya Wilaya 23;

(ii) Kufanya upimaji katika miradi ya kimkakati ya Bwawa la Mwalimu Nyerere lenye ukubwa wa Hekta 18,528.51; na Bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima hadi Chongoleani lenye urefu wa kilomita 1,147;

(iii) Kuimarisha mpaka wa Kimataifa wenye urefu wa kilomita 458 kati ya kilomita 758 za mpaka wa Tanzania na Kenya katika kipande cha nchi kavu;

(iv) Vijiji 975 kati ya 1975 vilivyoanzishwa ndani ya Hifadhi vimeidhinishiwa Ardhi jumla ya ekari 2,402,581.32 na kurudishwa kwa wananchi;

(v) Kuimarisha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa kuanzisha Mabaraza mapya 56 ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya na kufanya kuwa na jumla ya Mabaraza 111 yanayotoa huduma kati ya Mabaraza 139 yanayotakiwa kuwepo. Vilevile, Mashauri 93,873 yalitolewa maamuzi kati ya mashauri 107,823 yaliyokuwa yanashughulikiwa.

(l) Kuandaa Mipango 442 ya Matumizi ya Ardhi kwenye shoroba tatu za SGR, EACOP na TAZARA katika Wilaya 29 nchini. Aidha, Vijiji 1,133 vimeandaliwa Mipango ya Matumizi ya Ardhi, ambapo SGR (184), EACOP (207), JNHPP (148) na vijiji 594 katika maeneo mengine.

(m) Kuandaa na kuidhinisha Mipangokina 6,551 katika halmashauri nchini; Mipangokina 24 pembezoni mwa fukwe ya Bahari ya Hindi, Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria na Ziwa Nyasa; na kujenga Miji 21 ya kisasa (Setellite cities) katika mikoa ya Dar es salaam, Arusha, Dodoma, Mwanza na Tunduma.

5.1.2 Katika miaka mitano ijayo, CCM itahakikisha Serikali za Mitaa zinatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kufanya mageuzi makubwa ya kichumi, ili kutengeneza mazingira mazuri ya kujiajiri na kuajiriwa hususani kwa Vijana;

(b) Kufungamanisha miradi mikubwa ya kimkakati na shughuli za Wananchi kwenye Mitaa, Vijiji na Vitongoji ili waweze kunufaika na uwepo wa miradi hii mikubwa ya kimkakati;

(c) Kuendelea kuimarisha ujenzi wa miundombinu ya barabara, madaraja na vivuko katika Mitaa, Vijiji na Vitongoji ili kurahisisha upatikanaji wa huduma na kuimarisha uchumi wa wananchi katika maeneo yao;

(d) Kuendelea kuimarisha shughuli za uzalishaji kwenye kilimo, ufugaji na uvuvi ili kukuza uchumi wa kaya, usalama wa chakula na ustawi wa maisha ya wananchi;

(e) Kuendelea kuboresha maeneo ya biashara na uwekezaji ili kurahisisha shughuli za uwekezaji kwenye maeneo ya Mitaa, Vijiji na Vitongoji;

(f) Kuongeza kasi ya usambazaji umeme kwa gharama nafuu katika Mitaa na Vijiji vyote nchini ili kuchochea shughuli za kiuchumi na kuboresha maisha ya wananchi;

(g) Kuendelea kujenga na kuimarisha miundombinu ya matumizi ya gesi asilia ili kupunguza uharibifu wa mazingira na gharama za nishati. Serikali Kuuu itahakikisha kwamba lengo hili la matumizi ya nishati safi kwa wanawake linatekelezwa kwa kasi kubwa nchini kote na kupunguza kwa kiwango kikubwa matumizi ya kuni na mkaa. Misitu yetu itaanza kupona.

(h) Kuendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo kwa kuwapa mitaji, elimu na kuwatafutia teknolojia rahisi, rafiki na masoko ili kuongeza tija katika shughuli zao za uchimbaji na kuboresha maisha yao;

(i) Kuimarisha matumizi bora ya ardhi ya Vijiji kwa kutumia njia endelevu ikiwemo kuwashirikisha wananchi katika kutatua changamoto zilizopo kuendelea na urasimishaji wa ardhi na kujenga maridhiano katika jamii kwa kutumia mbinu mahsusi kama vile Mkakati wa "Tutunzane" unaotekelezwa katika Wilaya ya Mvomero;

(j) Kuendelea kupanga matumizi bora ya ardhi, kupima na kumilikisha ardhi kwa wananchi ili kuwawezesha kupata mikopo na motisha ya kuwekeza zaidi katika shughuli za kiuchumi hususan kilimo na ufugaji, pamoja na kupunguza migogoro ya ardhi na kulinda haki za watumiaji wote wa ardhi;

(k) Kuendelea kuandaa mipangokina ya maeneo ya makazi, malisho na kilimo katika vijiji, miji, visiwa na fukwe; pamoja na kuwezesha upatikanaji wa hatimiliki za kimila kwenye maeneo ya miradi ya kimkakati na maeneo ya mipakani;

(l) Kuendelea kurasimisha makazi yasiyo rasmi na kuyaboresha kwa huduma za kijamii na miundombinu ili kuwawezesha wananchi kunufaika na fursa za kiuchumi; pamoja na kufanya utambuzi wa miji midogo na miji inayokua kwa kasi na kuwezesha ujenzi wa miji ya kisasa;

(m) Kuendelea kutatua changamoto za wafanyabiashara wadogo kwa kuimarisha miundombinu katika maeneo yaliyotengwa;

(n) Kuendelea kuimarisha mifumo ya masoko ya mazao, mifugo na uvuvi pamoja na kuimarisha barabara zinazohusika katika usafirishaji wa mazao.

(o) Kuendelea kutenga na kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa makundi ya Vijana, Wanawake na Watu wenye Ulemavu ili kuongeza idadi ya Wananchi wanaojiajiri na kuajiri wengine, kuimarisha uwezo wao wa kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali na biashara; na

(p) Kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya kukuza na kuvutia uwekezaji katika sekta ya utalii kwa kutumia vivutio vinavyopatikana kwenye maeneo yao.

## 5.2 Maendeleo ya Watu

5.2.1 Katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Mwaka 2020 - 2025, Tanzania imewekeza katika nyanja zote na kufanikiwa kuwaletea maendeleo watu wake. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:-

| | | |
|---|---|---|
| 2020 2024 | **UJENZI** | |
| | Vituo vya Afya | **367** |
| | Maboma ya Zahanati | **980** |
| | **MABORESHO** | |
| | Majengo Huduma za Dharura | **28** |
| | **X-RAY** | |
| | Vituo vya Afya | **87** |
| | Hospitali za Halmashauri | **117** |

(a) Kuimarika kwa huduma za afya ambapo kuanzia 2020-2024 vituo vya afya vipatavyo 367 na maboma ya zahanati 980 yamejengwa kwenye maeneo ya Wananchi. Aidha, hospitali pia zimeboreshwa kwa ajili ya kutoa huduma za dharura ambapo majengo 28 yameboreshwa. Kuimarishwa kwa vituo vya afya kumehusisha kuongezeka kwa huduma za upasuaji; kusambazwa kwa X-ray 87 kwenye vituo vya afya na 117 kwenye hospitali za Halmashauri; kuimarisha upatikaji wa huduma za Bima ya Afya ambapo Wananchi wanaweza kutibiwa kuanzia zahanati, vituo vya afya mpaka hospitali za rufaa; kuboresha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi;

(b) Kuongezeka ufanisi katika afua za lishe ikiwemo huduma za lishe kwa wajawazito, wanawake wanaonyonyesha, watoto wachanga na wanafunzi;

(c) Kuongezeka kwa mikakati ya kupambana na udumavu na ukondefu katika jamii kwa watoto chini ya miaka mitano ikiwemo kuhamasisha lishe bora ya chakula mchanganiko kwa kuzingatia vyakula vinavyopatikana katika maeneo yao;

(d) Kufanikiwa kupunguza vifo vya wajawazito kutoka vifo 556 mwaka 2016 kwa kila vizazi hai 100,000 hadi kufikia vifo 104 mwaka 2022. Kupungua vifo vya watoto wenye umri wa chini ya miaka 5 kutoka vifo 67 kwa kila vizazi hai 1,000 hadi kufikia vifo 43 kwa kipindi hicho hicho;

**2016**
**2022**

VIFO VYA WAJAWAZITO

Kutoka **556**
Hadi **104**
kila Vizazi Hai **100,000**

---

VIFO VYA WATOTO
Chini ya Miaka **5**

Kutoka **67**
Hadi **43**
kila Vizazi Hai **1,000**



| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **2021 2024** | **UJENZI MPYA** | Msingi & Sekondari | **3,631** | |
| | | Madarasa | **21,912** | |
| | **UANDIKISHAJI WANAFUNZI** | darasa la awali | kutoka<br>hadi | **1,291,968**<br>**1,679,542** |
| | | shule za msingi | kutoka<br>hadi | **10,687,593**<br>**11,425,482** |
| | | sekondari | kutoka<br>hadi | **2,379,945**<br>**3,041,151** |

(e) Kuimarika kwa huduma za elimu ambapo mwaka 2021 hadi sasa jumla ya shule mpya za msingi na sekondari 3,631 zimejengwa na idadi ya madarasa mapya 21,912 yamejengwa. Serikali ya CCM imeendelea kutoa elimu bila ada kuanzia elimu ya awali mpaka kidato cha sita. Hii imechochea uandikishaji wa wanafunzi katika darasa la awali kutoka 1,291,968 mwaka 2021 hadi 1,679,542 mwaka 2024. Pia imechochea ongezeko la idadi ya wanafunzi wa shule za msingi kutoka 10,687,593 mwaka 2021 hadi 11,425,482 mwaka 2024, na sekondari kutoka 2,379,945 mwaka 2021 hadi 3,041,151 mwaka 2024;

(f) Kuimarika kwa shughuli za utamaduni, michezo na sanaa kama moja ya njia ya kujenga afya, kuongeza fursa za ajira na kipato; na

(g) Kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za maji katika Vijiji ambapo idadi ya Vijiji vilivyo na huduma ya maji safi na salama imefikia 9,259 sawa na asilimia 75.1 ya Vijiji vyote nchini (12,318) ambapo idadi ya Wananchi Vijijini wanaopata huduma ya maji safi na salama imefikia asilimia 77 mwaka 2023 na Mijini asilimia 88.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **2023 HUDUMA MAJI SAFI & SALAMA IMEFIKIA** | VIJIJI | **9,259** | **75.1%** | ya Vijiji **12,318** |
| | WANANCHI | Vijijini | **77%** | |
| | | Mijini | **88%** | |

5.2.2 Kuhusu huduma za jamii, CCM katika kipindi kijacho itahakikisha Serikali za Mitaa zinatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kusimamia upatikanaji wa huduma bora za afya karibu na Wananchi katika zahanati na vituo vya afya ikiwemo kuimarisha upatikanaji wa dawa, uweledi wa watoa huduma za afya na uimarishaji wa miundombinu;

(b) Kuendelea kuongeza ufanisi katika kutekeleza afua za lishe ili kupambana na utapiamlo, udumavu na vifo vya watoto chini ya miaka mitano;

(c) Kuendelea kuimarisha utoaji wa elimu ya msingi na elimu ya awali kwa kuboresha miundombinu yake na ukarabati wa shule kongwe za msingi na sekondari, kuimarisha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, madawati, matundu ya vyoo, maji safi na salama na upatikanaji wa chakula;

(d) Kuendelea kuboresha upatikanaji wa walimu mahiri wa kufundisha;

(e) Kuendelea kuweka mikakati ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi;

(f) Kuendelea kuimarisha shughuli za utamaduni, michezo na sanaa kama moja ya njia za kujenga afya, kuleta furaha kwenye jamii, kujenga mshikamano na kuongeza fursa za ajira na kipato;

(g) Kuendelea kuhakikisha kwamba huduma ya maji safi na salama inapatikana kwenye Vijiji na Mitaa yote nchini.

(h) Kuendeleza uchimbaji wa malambo ya maji ya mifungo, kuhimiza ufungaji bora inaojali wingi wa mifungo kwa eneo, upandaji wa majani bora ya mifungo, ujenzi wa majosho na upatikanaji wa kutosha wa dawa.

## 5.3 Utawala Bora, Haki, Ulinzi na Usalama

5.3.1 Uwepo wa utawala bora, haki, ulinzi na usalama ni muhimu kwa ajili ya ustawi wa jamii na maendeleo ya Nchi. CCM imekuwa ikihakikisha Taifa letu linazingatia misingi ya utawala bora, ulinzi wa haki za binadamu na uwepo wa usalama madhubuti kwa Wananchi na Taifa kwa ujumla. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:-

(a) Kuimarika kwa amani, utulivu na usalama nchini na hivyo kuwawezesha wananchi kushiriki kwa ukamilifu katika shughuli za kujiletea maendeleo bila bughudha;

(b) Kuhakikisha kuwa wananchi ndio walengwa wakubwa wa shughuli zote za Serikali katika ngazi zote;

(c) Kuimarisha mifumo ya kushughulikia haki za makundi maalum wakiwemo watu wenye ulemavu hususani ulemavu wa ngozi, masuala ya unyanyasaji wa kijinsia na watoto;

(d) Kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa, madawa ya kulevya, ubadhirifu wa mali za umma na matumizi mabaya ya madaraka katika ngazi zote;

(e) Kuimarisha mifumo ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao ikiwemo miundombinu na rasilimali muhimu katika maeneo yao;

(f) Kujenga jamii inayoheshimu na kuthamini utu,uwajibikaji, umoja, mshikamano wa kijamii, haki za binadamu, maadili mema, maridhiano na kustahimiliana.

5.3.2 Kuhusu Utawala Bora, CCM katika kipindi kijacho Itahakikisha Serikali za Mitaa zinatekeleza yafuatayo:-

(a) Utawala bora utaendelea kuwa nyenzo ya amani, utulivu, usalama na mshikamano katika jamii kwa kuweka mazingira mazuri ya wananchi kuendelea kufanya shughuli zao za maendeleo kwa tija na ufanisi;

(b) Utaendelea kuimarisha misingi ya utu, haki za binadamu, ushirikishwaji wa wananchi, demokrasia, uwajibikaji, uwazi na usawa katika jamii;

(c) Kuendelea kuhakikisha kuwa wananchi wanabaki kuwa msingi wa shughuli zote katika Mitaa, Vijiji na Vitongoji;

(d) Kuendelea kuweka mazingira rafiki ya kulinda haki za makundi maalum wakiwemo watu wenye ulemavu, masuala ya unyanyasaji wa kijinsia na watoto;

(e) Kuendeleza jitihada za mapambano dhidi ya rushwa, madawa ya kulevya, ubadhirifu wa mali za Umma na matumizi mabaya ya madaraka katika ngazi zote; na

(f) Kuendelea kujenga jamii inayozingatia misingi ya utu, umoja, mshikamano wa kijamii, haki za binadamu, maadili yetu, maridhiano na kustahimiliana.

## 5.4 Maendeleo ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi

5.4.1 Katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Mwaka 2020- 2025, Nchi imepata maendeleo makubwa katika sayansi, teknolojia na uvumbuzi kama nyenzo muhimu na ya haraka katika kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na :-

(a) Kuimarisha huduma za mawasiliano vijijini kwa kuhamasisha ujenzi wa minara, na kupunguza gharama za mawasiliano;

(b) Kuimarisha matumizi salama ya sayansi, teknolojia na uvumbuzi katika kutatua changamoto za wananchi, kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma kwa Wananchi kama vile elimu, afya, maji, na nishati; na

(c) Kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia za kidijitali ili kuongeza ufanisi katika sekta za uzalishaji na kuchangia ukuaji wa uchumi na kuboresha maisha ya Wananchi.

5.4.2 Katika kipindi kijacho, CCM itahakikisha Serikali za Mitaa zinatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika huduma zilizopo katika Serikali za Mitaa ikiwemo ukusanyaji wa kodi na maduhuli ya Serikali ili kuongeza uwazi na kuimarisha udhibiti wa makusanyo hayo;

(b) Kuendelea kuimarisha mazingira ya ukuaji wa matumizi ya teknolojia za kisasa na zinazoibuka kama vile Akili Mnemba (Artificial Intelligence), Bio teknolojia, Nano teknolojia katika kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma na shughuli za maendeleo kwa mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla;

(c) Kuhakikisha mfumo wa kidijiti unatumika kama nyenzo ya ukopeshaji wa asilimia 10 ya mapato ya ndani inayotumika kukopesha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwenye shughuli za uzalishaji mali katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kupitia miradi kama vile Jenga kesho iliyo bora (Building Better Tomorrow – BBT);

(d) Kuongeza ufanisi wa matumizi ya sayansi, teknolojia na uvumbuzi katika kutatua changamoto katika kutoa huduma za jamii.

(e) Kurahisisha upatikanaji wa mawasiliano na matumizi ya kidijiti katika Vijiji na Mitaa yote nchini.

## 5.5 Mazingira na Mabadiliko ya Tabia Nchi

5.5.1 CCM inatambua umuhimu wa kulinda na kutunza mazingira na kujenga uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Katika kipindi cha mwaka 2020 – 2025, mafanikio mengi yamepatikana yakiwemo:-

(a) Kuanzisha na kuanza kutekeleza mkakati wa miaka 10 wa matumizi ya nishati safi na salama ya kupikia ambao utahakikisha kwamba asilimia 80 ya Watanzania ifikapo 2034 wawe wanatumia teknolojia hii;

(b) Kuimarisha usimamizi na uhifadhi wa mazingira na uwezo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi. Aidha, Kusimamia kampeni ya usafi wa mazingira katika maeneo ya Serikali za Mitaa.

(c) Kupunguza matumizi ya taka ngumu ikiwemo mifuko ya plastiki ili kulinda mazingira; na

(d) Kupanda na kustawisha miti zaidi ya Milioni 200 katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kama moja ya njia ya udhibiti wa hewa ya ukaa.

5.5.2 Katika kipindi kijacho, CCM itahakikisha Serikali za Mitaa zinatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuimarisha uwezo wa Serikali za Mitaa katika usimamizi na uhifadhi wa Mazingira ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabian-chi;

(b) Kuendelea kusimamia usafi wa mazingira ikiwemo kuweka miundombinu ya kukusanya, kuhifadhi na kuchakata taka za aina zote katika maeneo ya Mitaa, Vijiji na Vitongoji;

(c) Kuendelea na kampeni za kupanda, kustawisha miti na Misitu kwenye Mitaa, Vijiji na Vitongoji ili kudhibiti hewa ukaa na kuongeza uwezo wa vijiji kupata maduhuli;

(d) Kuendelea na kampeni ya usafi wa mazingira katika maeneo yaliyo chini ya Serikali za Mitaa; na


(e) Kuhakikisha matumizi endelevu ya maliasili zilizopo katika Mitaa, Vijiji na Vitongoji kwa ajili ya faida ya vizazi vya sasa na vijavyo kama vile kuhifadhi afya ya udongo, vyanzo vya maji, makazi ya asili ya wanyamapori na viumbe hai wengine.









SU 42274





# 6.0 HITIMISHO

6.1 CCM inatambua umuhimu wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kwamba Serikali hizi ndio injini ya maendeleo ya nchi hivyo zinahitaji kupata viongozi wazuri, wenye weledi, waadilifu na wanaokubalika kwa wananchi. Hivyo tamko hili litatumika kuhakikisha viongozi wa aina hiyo wanapatikana.

6.2 CCM inatambua kwamba, hatua ya kuzitambua na kuziainisha fursa zilizopo kwenye maeneo ya wananchi ili zitumike kuboresha maisha yao na kuchangia katika maendeleo ya jamii zinapaswa kuendana na mikakati endelevu, uongozi imara na utashi wa kisiasa katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali za Mitaa.

6.3 Hivyo, kwa kushirikiana na Wananchi wenyewe kwenye maeneo yao, na kwa kupitia Serikali zao za Mitaa, CCM imejizatiti kikamilifu kimuundo na kiuongozi, kutumia rasilimali zilizopo pamoja na fursa zilizopo ili kufanikisha shughuli za utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020 – 2025 kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

6.4 Pamoja na maelekezo yote yaliyopo kwenye Tamko hili, wagombea wanaelekezwa kubainisha na kueleza miradi na shughuli ambazo zimefanywa na Serikali ya CCM na kuzieleza kikamilifu kwa Wananchi. Aidha, wagombea wote wanaelekezwa kubainisha fursa zilizopo katika nyanja zote – Kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa kwa ajili ya kushirikiana na Wananchi kuzitumia kwa ustawi na maendeleo ya Wananchi na jamii zao.

6.5 Katika kutekeleza dhamira yake hiyo na kwa kupitia Tamko hili , CCM inapenda kuwaomba na kuwasihi Watanzania wote, hususan walio na sifa ya kupiga kura wakati utakapofika, kujitokeza kwa wingi kwenda kujiandikisha na siku ya uchaguzi kupiga kura zao za NDIO, kwa wagombea wa CCM watakaoteuliwa kugombea nafasi za Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji, Wajumbe wa Kamati za Mitaa na Wajumbe wa Halmashauri za vijiji katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024.

# KIDUMU CHAMA CHA MAPINDUZI

*Tumetekeleza,*
*Kazi Iendelee...*

CHAMA CHA MAPINDUZI

LENGA KAMERA KUPAKUA

CHAMA CHA MAPINDUZI

**IMETOLEWA NA;**
Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.